## Wanaume, Wanawake na Usawa wa

Biblia hufundisha kikamilifu usawa kati ya mwanaume na mwanamke wakati wa uumbaji na ukombozi (Mwa 1:26-28, 2:23, 5:1-2; 1Kor 11:11-12; Wag 3:13, 28, 5:1).

Biblia hufundisha kwamba Mungu mwenyewe alijifunua kupitia ukamilifu wa maandiko, katika mamlaka ya neno lake (Math 5:18; Yoh 10:35; 2Tim 3:16; 2Petro 1:20-21). Tunaamini kwamba maandiko yanapaswa kutafsiriwa kihistoria na kutokana na Mada. Pia tumetambua umuhimu wa kuweka tofauti kati ya msukumo na tafsiri: msukumo unahusiana na mvuto wa kimugu na udhibiti wa neno, lakini tafsiri yake ni uthibitisho rasmi, usio na mashaka wa maandiko kuwa ni neno la Mungu. Tafsiri ya neno inahusiana na shughuli za moja kwa moja za wanadamu ambapo tunatafuta kuelewa kweli iliyo wazi ya neno la Mungu katika ulinganifu kwa jumla wa maandiko kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Wakristo ili wawe na uelewa mzuri wa maandiko, wanalazimika kuendelea kuchunguza na kuitendea kazi Imani yao katika mwangaza wa kuyachunguza maandiko matakatifu.

**UKWELI WA KIBIBLIA**

**<u>Uumbaji</u>**

1. Biblia inafundisha kwamba, mwanamke na mwanaume wote waliumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, walikuwa na ushirika wa moja kwa moja na Mungu, na walishirikiana kwa pamoja katika majukumu ya uzazi na malezi ya watoto, na kuitawala dunia na vyote vilivyoumbwa (Mwa 1:26-28)
2. Biblia inafundisha kwamba, mwanamke na mwanaume waliumbwa katika utimilifu na usawa katika kushirikiana. Neno “msaidizi” (Ezer) lililotumika kumtambulisha mwanamke hutumiwa zaidi kama rejea kumwakilisha Mungu katika maandiko ya Agano la kale. (Mf: 1Sam 7:12; Zab 121:1-2). Kwa hivyo, neno hilo halileti maana yoyote linapotumika kuonyesha unyonge na uduni wa mwanamke.
3. Biblia inafundisha kuwa, kuumbwa kwa mwanamke kutoka kwa mwanaume ni ishara inayoonyesha msingi wa umoja na usawa wa binadamu wote. (Mwa 2:21-23). Katika kitabu cha Mwa 2:18 neno “wa kufanana nae” (Kenegdo) linaashiria usawa na utoshelevu.
4. Biblia inafundisha kwamba, mwanamke na mwanaume wote walishiriki katika anguko: Adam naye alikuwa na hatia kama Eva. (Mwa 3:6; Warumi 5:12-21; 1Kor 15:21-22).
5. Biblia inafudisha kuwa, hali ya Adam kumtawala Eva ilikuwa ni matokeo ya anguko, haukuwa mpango wa awali wa Mungu wakati wa uumbaji. Mwanzo 3:16 ni utabiri wa madhara ya anguko badala ya mpango mkamilifu wa Mungu wakati anaanza kuumba.

**<u>Ukombozi</u>**

6. Biblia inafundisha kuwa Yesu Kristo alikuja kuwakomboa wanawake na wanaume pia. Kwa Imani kupitia Yesu Kristo, wote tunafanyika kuwa watoto wa Mungu, na warithi wa Baraka za wokovu bila kujali rangi, tofauti za kijamii au kijinsia. (Yohana 1:12-13; Warumi 8:14-17; 2Kor 5:17; Wagalatia 3:26-28)

**Katika Jamii**

7. Biblia inafundisha kwamba, siku ya Pentekoste,  Roho Mtakatifu aliwashukia wote wanaume na wanawake. Bila ubaguzi, Roho Mtakatifu hukaa ndani ya wanawake na wanaume na kwa mamlaka yake hugawa vipawa bila upendeleo wa kijinsia. (Mdo 2:1-21; 1Kor 12:7, 11, 14:31).
8. Biblia inafundisha kwamba, wanawake na wanaume wote wameitwa kuendeleza na kukuza vipawa vyao vya Rohoni na kuvitumia kama mawakili wa neema ya Mungu. (1Petro 4:10-11). Wote wanawake kwa wanaume wamepewa vipawa na uwezo wa kiungu ili kuutumikia mwili wa Kristo chini ya mamlaka yake. (Mdo 1:14, 18:26, 21:9; Warumi 16:1-7, 12-13, 15; Wafilipi 4:2-3; Wakolosai 4:15; pia tazama Marko 15:40-41, 16:1-7; Luka 8:1-3; Yohana 20:17-18; linganisha pia mifano ya agano la kale Waamuzi 4:4-14, 5:7; 2Nyakati 34:22-28; Mithali 31:30-31; Mika 6:4).
9. Biblia inafundisha kwamba, katika mazingira ya agano jipya, wanamume na wanawake walidhihirisha vipawa vyao katika unabii, ukuhani na huduma za kifalme. (Mdo 2:17-18, 21:9; 1Kor 11:5; 1Petro 2:9-10; Uf 1:6, 5:10). Kwa hiyo, maandiko machache yaliyotengwa yanayozungumzia kuzuia ukombozi kamili na uhuru wa wanawake yasitafsiriwe kirahisi na kinyume na maandiko yote ya biblia, tafsiri za maandiko hayo ni lazima zizingatie uelewa mpana wa mafundisho hayo na mazingira yake. (1Kor 11:2-16, 14:33-36; 1Tim 2:9-15)
10. Biblia inatafsiri maana na kazi ya uongozi kuwa ni kuwawezesha watu wengine ili waweze kufanya kazi zao, maana na kazi ya uongozi si kutumia mamlaka dhidi ya watu wengine. (Mat 20:25-28, 23:8; Marko 10:42-45; Yoh 13:13-17; Wagalatia 5:13; 1Petro 5:2-3).

**Katika Familia**

11. Biblia inafundisha kwamba waume na wake wote ni warithi wa neema ya uzima na wameunganishwa katika uhusiano kwa kuonyesha unyenyekevu na uwajibikaji wa pamoja. (1Kor 7:3-5; Waefeso 5:21; 1Petro 3:1-7; Mw 21:12). Kazi kuu ya mume kama "kichwa" (Kephale) cha familia ieleweke kuwa ni kujitoa kwa kuonyesha upendo na kuwahudumia wale anaohusiana nao kwa unyenyekevu. (Waefeso 5:21-33; Wakolosai 3:19; 1Petro 3:7).
12. Biblia inafundisha kwamba baba na mama kwa pamoja wanatakiwa kuongoza au kuonyesha njia katika malezi, nidhamu na mafundisho kwa watoto wao. (Kut 20:12; Walawi 19:3; Kumb 6:6-9, 21:18-21, 27:16; Mith 1:8, 6:20; Waefeso 6:1-4; Wakolosai 3:20; 2Tim 1:5; tazama pia Luka 2:51).

**UTEKELEZAJI**

**Kijamii**

1. Katika kanisa, vipawa vya Rohoni vya wanawake na wanaume vinapaswa kutambuliwa, kuendelezwa na kutumiwa katika kufundisha kwenye huduma mbalimbali katika ngazi zote za ushiriki: kuanzia uongozi wa makundi madogo, washauri, wawezeshaji, watawala, mashemasi, watoa huduma ya sakramenti ya meza ya Bwana, na wanachama wa bodi, na katika huduma za kichungaji, kufundisha, kuhubiri na kuabudu.

Kwa kufanya hivyo, kanisa litakuwa limemtukuza Mungu kama mtoaji na mgawaji wa vipawa vya Rohoni. Kanisa litakuwa pia limetimiza mamlaka ya Mungu kwa uwakili usio na mawaa na bila kuleta hasara kwenye ufalme wa Mungu, hasara ambayo itatokea ikiwa nusu ya wamumini watabaguliwa kutoka na jinsia katika nafasi zao za majukumu.

2. Katika kanisa, utambulisho kwa wanawake na wanaume wanaotoa huduma na uongozi ufanyike kwa wote bila kutoa upendeleo wa kijinsia.

   Kwa kufanya hivyo, kanisa litakuwa mfano wa umoja na maelewano ambayo ndio msingi na sifa ya jamii ya waaminio. Katika dunia iliyoharibiwa na ubaguzi na matengano, kanisa litakuwa limejiondoa toka mfumo wa kidunia na kipagani uliotengenezwa ili kuwafanya wanawake wajisikie duni kwa kuwa wao ni wanawake. Itasaidia kuzuia wanawake kuondoka makanisani au kuikataa Imani ya Kikristo.

**<u>Kifamilia</u>**

3. Katika familia za kikristo, mume na mke wanatakiwa kuridhianakatika kutafuta kutimiza matamanio, matarajio na malengo ya kila mmoja. Mwanandoa yeyote hatakiwi kutafuta kumtawala mwenzake bali kila mmoja awe kama mtumwa kwa mwenzake, kwa unyenyekevu huku kila mmoja akimuona mwenzake kuwa bora kuliko yeye. Wakati wa msuguano wa kimaamuzi, wanatakiwa kutafuta suluhisho kwa kufuata utaratibu wa kibiblia wa kutatua misuguano badala ya mwanandoa mmoja kulazimishia suluhisho lake dhidi ya mwenzake.

   Kwa kufanya hivyo, mume na mke watasaidia nyumba za kikristo kusimama kinyume cha matumizi mabaya ya nguvu na mamlaka kwa wanandoa na pia itawalinda wanawake na watoto kuepukana na ukatili, jambo ambalo wakati mwingine husababishwa tafsiri mbaya na hatarishi za “mwanaume kuwa kichwa cha familia”

4. Katika familia za kikristo,wanandoa wajifunze kushirikiana majukumu ya uongozi kwa misingi ya vipawa, utaalamu, na upatikanaji unaozingatia kumjali yule anayeathirika zaidi na maamuzi.

   Kwa kufanya hivyo, wanandoa watajifunza kuheshimu uwezo wao na kusaidiana. Hii itamsaidia mwanandoa mmoja kuepukana na hali ya kushindwa daima, au kulazimishwa kufanya mambo kinyume kwa ajili tu ya kulinda heshima yake. Kwa kujenga ndoa zao katika misingi ya ushirikiano, wanandoa watakua wameiepusha ndoa yao na wimbi la ndoa mfu au ndoa zinazovunjika kutokana na kutokuwepo na usawa wa kijinsia.

5. Katika familia za kikristo, wanandona washiriki mfumo wa maisha yalio na uhuru unaopatikana ndani ya Kristo, watafanya hivyo bila kujisikia hatia au kutenda kwa unafiki.Watakuwa wamewekwa huru toka mila zisizofuata neno la Mungu (Biblia), nawatafurahia umoja na uwajibikaji wao ndani ya Kristo. Kwa kufanya hivyo, wataweza kuelezea kwa uwazi kabisa juu ya utiifu wao wa neno la Mungu, na kuwa mfano kwa wanandoa wengine wanaojitahidi kuishi

maisha ya uhuru ndani ya Kristo na kusimama kinyume cha mfumo wa kutokuwepo na usawa unaoletwa wakati mwingine na familia au kanisa.

*Tunaamini kwamba usawa wa kibiblia kama ulivyooneshwa kwenye hati hii ni kweli kwa mujibu wa maandiko.*

*Tunaungana katika Imani kwamba biblia kwa ujumla wake ni neno la ukombozi linalotupa njia iliyo sahihi zaidi kwa wanawake na wanaume kutumia vipawa vyao walivyopewa na Roho Mtakatifu ili kumtumikia Mungu.*

**Christians for Biblical Equality**
122 West Franklin Avenue, Suite 610,
Minneapolis, MN 55404-2426
Phone: **(612) 872-6898**
Email: **cbe@cbeinternational.org**
**www.cbeinternational.org**